
WIZARA YA MAJI

BODI YA MAJI BONDE LA WAMI/RUVU

# UTABIRI WA HALI YA WINGI WA MAJI KATIKA MTO RUVU KWA KIPINDI CHA MEI - JULAI 2025







Imeandaliwa na;

**Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu**


**P.O. Box 826, Morogoro—Tanzania**

**Phone:** 0800114031 / 0800114032

**E-mail**: barua@wrbwb.go.tz

**Website**: www.wrbwb.go.tz


**Aprili, 2025**

# 1. UTANGULIZI

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu imeandaa na kuwasilisha utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kipindi cha Mwezi Mei hadi Julai,2025 ili wadau wa Mto Ruvu katika sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Viwanda, Utalii na Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira waweze kuchukua tahadhari na hatua zaidi dhidi ya upungufu wa wingi wa maji unaoweza kujitokeza. Utabiri unaonyesha kupungua kwa wingi wa maji kutoka wastani wa juu hadi kufikia chini ya wastani kutokana na uhaba wa mvua katika safu ya Milima ya Uluguru katika kipindi cha Mwezi Mei- Julai, 2025[1], hali hii inaweza kupelekea upungufu wa upatikanaji wa maji katika shughuli za kijamii na kiuchumi hasa kuanzia kipindi cha Mwezi Julai, 2025.

## 1.1 ATHARI ZINAZOWEZATOKEA

Uhaba wa maji kwa sekta tajwa kutokana na kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu hasa kuanzia Mwezi Julai 2025


[1] Taarifa ya Mwelekeo wa Mvua za masika zilizotolewa Mwezi Aprili, 2025 na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania


## 2. UTABIRI WA HALI YA MAJI

Utabiri wa hali ya wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kipindi cha Mwezi Mei hadi Julai, 2025 unaonyesha kiasi cha wingi wa Maji kitapungua kutoka mita za ujazo 242 kwa sekunde katika kipindi cha Mwezi Mei hadi kufikia mita za ujazo 15 kwa sekunde Mwezi Julai (**Jendwali Na.1)**. Hali hii itapelekea wingi wa maji katika Mto Ruvu kuwa juu ya wastani Mwezi Mei 2025 hadi kufikia chini ya wastani Mwezi Julai 2025 ukilinganisha na wastani wa muda mrefu (2009-2024). Hatahivyo, utabiri unaonyesha hali ya upatikanaji wa wingi wa maji utakuwa stahilifu unaotosheleza mahitaji ya sekta mbalimbali ambayo ni mita za ujazo 6 kwa sekunde.

Aidha, utabiri unaonyesha kwa kipindi cha Mwezi Mei hadi Julai 2025 ujazo wa maji katika Mto Ruvu utakuwa mita za ujazo milioni 489, ujazo huu utakuwa unakaribia ujazo wa Mwaka 2014-2015 ambapo hali ilikuwa wastani ukilinganisha na Mwaka 2020-2021 na 2021-2022 ambapo kulikuwa na uhaba mkubwa wa upatikanaji wa maji katika Mto Ruvu.

**Jendwali Na. 1: Utabiri wa hali ya wingi wa maji Mto Ruvu katika kituo cha *Ruvu river at* Morogoro road bridge (1H8A).**

| Jina la Mto | Utabiri wa Hali ya Wingi wa Maji | Kielelezo |
|---|---|---|
| *Ruvu river at Morogoro road bridge (1H8A)* | Utabiri unaonyesha kupungua kwa wingi wa maji kutoka wastani wa juu hadi kufikia chini ya wastani ukilinganisha na wastani wa muda mrefu. Aidha, kupungua kwa wingi wa maji katika Mto Ruvu utatokana na kupungua kwa mvua katika safu ya Milima ya Uluguru, hali hii inaweza kupelekea upungufu wa upatikanaji wa maji katika shughuli za kijamii na kiuchumi hasa katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2025 (**Kielelezo**). |  |

| | | |
|---|---|---|
| | Utabiri unaonyesha kwa kipindi cha Mwezi Mei hadi Julai 2025 ujazo wa maji katika Mto Ruvu utakuwa mita za ujazo milioni 489, ujazo huu utakuwa unakaribia ule ujazo wa Mwaka 2014-2015 ambapo hali ilikuwa wastani ukilinganisha na Mwaka 2020-2021 na 2021-2022 ambapo kulikuwa na uhaba mkubwa wa upatikanaji wa maji katika Mto Ruvu. |  |

## 3. USHAURI

Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu inazishauri sekta za Kilimo, Madini, Utalii, Ufugaji na Uvuvi, Viwanda na usambazaji maji majumbani kuzingatia mambo yafuatayo; -

### a) Mamlaka za Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mjini (UWSSA) na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA)

Bodi inazishauri Mamlaka na Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira kuwekeza katika uchimbaji na kuendeleza visima virefu vilivyochibwa katika maeneo mbalimbali ili kukabiliana na uhaba wa maji Mtoni unaoweza kujitokeza kuanzia Mwezi Julai,2025.

### b) Kilimo

Bodi inasisitiza wakulima kutumia maji kwa ufanisi zaidi kwa kuzuia upotevu wa maji katika mashamba yao na kuhakikisha mifereji imejengewa, pia kuyarudisha maji Mtoni pindi wanapomaliza kuyatumia. Aidha, wakulima wanashauriwa kuzingatia ushauri wa Maafisa Kilimo juu ya umwagiliaji wa mazao katika maeneo yao kwa kuzingatia kalenda ya umwagiliaji na kuzuia umwagiliaji wa kila siku ili watumiaji wengine waliopo chini waweze kunufaika. Pia, Bodi inawataka wakulima kuchepusha maji kutoka mtoni kama yalivyoanishwa katika vibali vyao vya matumizi ya maji. Sekta ihakikishe inaweka kipaumbele katika ujenzi wa miundombinu ya mabwawa ya kimkakati ili yaweze kutumika kipindi cha kiangazi ambapo kunakuwa na uhaba wa maji Mtoni.

### c) Ufugaji na Uvuvi

Bodi inashauri sekta kuhakikisha mifugo zinanyweshwa katika maeneo yaliyotengwa na kujengewa mabirika, pia Halmashauri za Wilaya kuhakikisha mifugo zinalishwa katika maeneo yaliyoanisha katika mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuepusha uchafuzi na uharibifu wa vyanzo vya maji. Aidha, uvuvi wa kutumia sumu na kuweka vizuizi katika vyanzo vya maji hauruhusiwi.

### d) Madini

Bodi inashauri Sekta ya Madini na Halmashauri za Wilaya kuhakikisha uchimbaji na uchejuaji wa Madini unafanyika nje ya vyanzo vya maji ili kulinda ubora wa maji.

### e) Utalii

Kina cha maji kuanzia Mwezi Julai 2025 kitaanza kupungua hali itakayoathiri makazi ya Wanyama waishio majini wakiwemo Viboko, Mamba na Samaki, hivyo Bodi inashauri sekta kufuatilia kwa ukaribu mwenendo wa maisha ya wanyama hao kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Mei 2025.

## 4. HITIMISHO

Bodi itaendelea kufuatilia na kuwahabarisha Wadau wake juu ya utabiri huu wa mwenendo wa wingi wa maji katika Mto Ruvu kwa kutoa utabiri kila baada ya siku kumi ili wadau waendelea kuchukua hatau za tahadhari dhidi ya upungufu wa wingi wa maji utakaoweza kujitokeza kwa siku zijazo.